TARGETER WINGS

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

GREDI 4 - 2021

Wings 005

SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina .....

Jina la shule .....

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Viwango vya kutathmini			
	Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
Kusikiliza na Kuzungumza	5 ☐	3 - 4 ☐	3 ☐	0 - 2 ☐
Kusoma kwa sauti	Maneno 71 na zaidi ☐	Maneno 51-70 ☐	Maneno 25 - 50 ☐	Maneno 0 - 24 ☐
Sarufi	19 - 20 ☐	13 - 18 ☐	6 - 12 ☐	0 - 5 ☐
Ufahamu	9 - 10 ☐	6 - 8 ☐	3 - 5 ☐	0 - 2 ☐

SEHEMU YA KWANZA

I. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu asome hadithi hii mwanafunzi akisikiliza kisha amwulize maswali.

KIHOTO, SHULE YANGU

Kihoto ni shule nzuri. Ina madarasa makubwa na walimu wazuri. Ina bustani la maua ya kupendeza. Ina kiwanja kikubwa cha kuchezea. Ina maktaba yenye vitabu vya hadithi tamu. Ina ua ambao umeizunguka ili kulinda usalama wa wanafunzi. Shule hii huwa namba moja katika michezo.

a) Taja shule inayozungumziwa katika hadithi. *(Mwanafunzi ajibu)*

b) Taja vitu mbalimbali vinavyopatikana katika shule hii. *(Mwanafunzi ajibu)*

c) Ni nini inapatikana kwenye maktaba ya shule hii? *(Mwanafunzi ajibu)*

d) Shule hii imezingirwa na nini? *(Mwanafunzi ajibu)*

e) Shule hii inaongoza katika nini? *(Mwanafunzi ajibu)*